**JINA: ………………….………………NAMBARI: ……….. KIDATO: …………**
**KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**
**MACHI MWAKA 2021**

**UFAHAMU ( ALAM 15)**

Rita na Evelyn walikuwa marafiki wa chanda na pete kwa muda mrefu. Waliishi katika mtaa wa Kibokoni jijini Mombasa. Evelyn alikuwa mwanafunzi wa masomo ya uhazili katika chuo kimoja pale mjini. Naye Rita alifanya kazi ya ukarani papo hapo mjini. Waliishi kidugu katika chumba kimoja walichopanga pale mtaani.

Ingawa marafiki hawa walishirikiana kwa kila njia katika shughuli za upishi, kupiga deki, kufagia, kufua na kazi nyinginezo za nyumbani, aliyekuwa akitoa msaada mkubwa zaidi alikuwa ni Rita. Rita alikuwa na mazoea ya kutunza pesa zake vyema. Aidha alijua maana ya haba na haba hujaza kibaba. Alijua kuwa Evelyn, kama mwanafunzi, hakuwa na uwezo wa kuyakidhi baadhi ya mahitaji yake. Alijitolea sabili hata kumnunulia Evelyn nguo, viatu na vim vingine alivyohitaji. Mara nyingine ilibidi Rita kulipa kodi ya nyumba peke yake kwa vile mwenzake hangeweza kupata pesa kwa wakati. Hakuwahi hata siku moja kumkera wala kumtesa Evelyn kwa jinsi yoyote ile. Fauka ya hayo, hakuwahi kumsemesha vibaya wala kuonyesha dharau kwake. Aliamini kama wanavyosema watu kuwa dunia rangi rangile, huenda siku moja atahitaji kusaidiwa yeye pia. Siku kama hiyo atamtegemea Evelyn, mwandani wake.

Evelyn alipomaliza masomo yake alikuwa na bahati ya mtende. Alipata kazi nzuri mara moja katika kampuni moja ya maffita papo hapo jijini. Lakini muda si muda, mambo ya ajabu yalianza kutokea. Baada ya kupata kazi yenye kipato kizuri, kichwa cha Evelyn kilianza kufura mfano wa kaimati. Badala ya kunisaidia mwenzake katika kazi za pale nyumbani pamoja na gharama za maisha, alifhatilia raha za jijini kwa kuamini ule msemo wa ponda raha kufa kwaja. Rita alipomwuliza alimjibu kwa ukali, “Nikusaidie nini? Sasa si kama wakati nilipokuwa mwanafunzi. Kila mtu ana pesa zake.Ala!”

Rita hakumwelewa tena Evelyn.Isistoshe, alianza kumwibia Rita vitu vyake wakati alipokuwa hayupo nyubani. Mara kwa mara Rita aligundua kuwa pesa alizokuwaameficha sehemu Fulani nyumbani zimedokolewa. Alipomwuliza, Evelyn alikujajuu, “Unafikiri mimi sina pesa? Unadhani ni wewe tu uliyeajiriwa?” Rita alizidi kushangaa, Muda wote alioishi na kumfadhili rafiki yake aliamini kuwa atamlipa mema. “Kumbe fadhila za punda ni mateke?” Alijiuliza Rita. Baada ya muda, urafiki wao ulivunjika na Evelyn akahamia mtaa wa Furaha alikoendelea na maisha yake ya starehe na ureda.

Hata hivyo mambo yalianza kumwendea mrama Evelyn. Wakubwa wake kazini hawakupendezwa najinsi alivyoendesha shughuli zake pale ofisini. Mara nyingi alifika kazini akiwa amechelewa na kila wakati alitoa vijisababu mbalimbali ambavyo havikumridhisha yeyote. Aidha, alipokuwa ofisini hakufanya mengi

isipokuwa kutembea kutoka ofisi hii hadi nyingine akiwasumbua watu kazini mwao. Mara kwa mara alionekana akisinzia wakati wenzake walipokuwa wakichapa kazi. Lakini lililowakera zaidi wakuu wa kampuni hiyo ya mafuta ni jambo fulani lililoanza kutendeka pale. Vitu vya watu vilianza kupoteapotea.Mara mfanyikazi huyu anapoteza saa yake, mara mwingine anapoteza pesa, mara hiki mara kile. Wakuu walipoyatupa mawazo yao nyuma wakagundua kuwa mambo haya yalianza kutendeka mara tu alipowasili Evelyn. Wakaamua kumwekea mtego. Evelyn alioshikwa kimasomaso akidokoa mkoba wa msichana mwenzake. Mkoba huo ulikuwa umeaehwa juu ya dawati kimakusudi ili kumvuta Evelyn. Evelyn alifutwa kazi papo hapo. Fauka ya hayo, alitiwa mikononi na kukabidhiwa poisi waliomtupa korokoroni. Kesho yake Evelyn alifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la wizi. Alitozwa faini ya shilingi elfu tano au kifungo cha miezi sita. Hakuwa na pesa zozote za kulipia faini hii. Akawekwa rumande. Hata rafiki mmoja hakuwa naye wa kumuauni katika wakati huo wa majaribu.

Kwa bahati, Rita alisikia kuhusu kadhia hiyo.Hakupoteza muda. Akashika njia moja kwa moja hadi kituo cha polisi. Mpango ukafanywa na akamlipia. Evelyn ile faini. Evelyn alipoachiliwa hum akashangaa. “Yaani nimesamehewa ama nini?”Aliuliza.“La. Hujasamehewa.Faini uliyotozwa imelipwa na msichana yule.” Evelyn akageuka na kumwona Rita. Alimtazama kwa muda bila kujua la kusema. Mwishowe alimsogea kisha wakakaribiana polepole na kukumbatiana. Machozi yakaanza kumdondoka Evelyn, nde! Nde! Nde! Akalia kilio cha uchungu na soni. Akamwomba Rita msamaha, “Nisamehe, sikujua nililokuwa nikifanya.Nilidhani kuwa baada ya kupata kazi sitahitaji tena urafiki wako. Haya yaliyonipata yamenifunza,” alisema kwa masikitiko. “Evelyn, kijengacho mtu ni uth na tabia,” alisema Rita.“Ni kweli rafiki yangu” alitamka Evelyn, Sasa nimejitia kwenye shida.Hata kazi yangu nzuri nimeipoteza.Sina mahali pa kuishi. Itabidi nirudi kijijini kwa baba na mama. Kwaheri rafiki yangu naasante kwa yote uliyofanya.”“La! Hutaondoka”. Rita alimwambia lcwa dhati, “Tutakwenda nawe nyumbani mwangu tukaishi pamoja kama zamani. Nitayagharamia mahitaji yako yote hadi utakapopata kazi”.

Basi Rita na Evelyn wakaungana tena na kuishi vizuri katika nyumba ile ile mtaani Kibokoni. Kweli akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

MASWALI:

1. Maisha ya Evelyn na Rita yalikuwaje kabla ya Evelyn kupata kazi? (alama 2)

______________________________________________________________

________________________________________________

2. Kutokana na jinsi Rita alivyomtunza Evelyn, unafikiri yeye alikuwa ni mtu wa ama gani? (alama 2)

______________________________________________________________

________________________________________________

3. Eleza baadhi ya mambo ambayo Rita alimtendea mwenzake. (alama 2)

_______________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Baada ya kupata kazi Evelyn alikuwa mtu mkarimu. Je, unakubali?Eleza ilivyokuwa. (alama 2)

_______________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

5. Evelyn alipokuwa mwanafunzi hakuwa na tabia ya udokozi. Unafikiri ni kwa nini alianza tabia hiyo baada ya kuajiriwa? (alama 2)

_______________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

6. 'Asiyefunza na mama hufunzwa na ulimwengu.' Methali hii inahusianaje na Evelyn? (alama 1)

______________________________________________________________________________

7. 'Akufaaye kiwa dhiki ndiye rafiki.' Methali hii inahusianaje na Rita? (alama 1)

______________________________________________________________________________

8. Eleza maana ya misemo ifuatayo kama ilivyotumika kwenye kifungu: (alama 3)

(a) marafiki wa chanda na pete

_______________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________

(b) enda mrama

_______________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

(c) jitolea sabili

_______________________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ( ALAMA 35)

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au sighuna. (al 2)
   (i) /t/

   (ii) /g/

2. Kamilisha methali zifuatazo; (al 2)

   (i) Mgaagaa na upwa ________________________________________________
   (ii) Mvumilivu______________________________________________________________

3. Andika visawe vya ; (al 2)
   (i) Janibu

   (ii) Jadi

4. Tunga sentensi zenye maneno yafuatayo; (al 3)
   (i) N + V + T

   (ii) N + V + T + E

   (iii) I + N + T

5. Onyesha viambishi awali na tamati katika sentensi hizi; (al 2)
   (i) Alimkaribisha

   (ii) Umeogelea

6. Onyesha matumizi manne ya koma. (al 4)

7. Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? (al 3)
   (i) Mchungwa
   (ii) Mdudu
   (iii) Bonde

8. Andika sentensi zifuatazo katika umoja. (al 3)
   (i) Nyavu zimechanikachanika

   (ii) Nyuzi ziliingia matata

(iii) Fito zilikatwakatwa

9. Andika wingi wa; (al 3)
   (i) Kiganja
   (ii) Cheo
   (iii) Kibindo

10. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao. (al 2)
   (i) Mimi ninapenda mtoto mtiifu.

   (ii) Ninyi mnapendwa na wenzenu.

11. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali timilifu. (al 2)
   (i) Safari hii itakuwa ndefu

   (ii) Shamba letu linalimwa

12. Tunga sentensi ukitumia vitenzi hivi katika hali ya kutendewa. (al 2)
   (i) Kata

   (ii) Pasua

13. Eleza maana ya kirai. (al 1)

14. Onyesha kundi Nomino na kikundi tenzi katika sentensi hii. (al 2)

   Hatibu hupaswa kuifahamu lugha

15. Tegua vitendawili vifuatavyo. (al 2)
   Kisima kidogo kimejaa changararwe

Namsikia lakini simwoni

**ISIMU JAMII (Al 10)**

(i) Eleza maana ya sajili ya shuleni. (al 2)

(ii) Taja sifa nane za sajili ya shuleni. (al 8)

**FASIHI SIMULIZI AL 10**

1. (a) Fafanua maana ya ; (al 2)
    (i) Fasihi andishi

    (ii) Fasihi simulizi

    (b) Onyesha tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. (al 8)